JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

# MAJUKUMU YA OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA

## Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inatekeleza majukumu yafuatayo:-

i. Kusajili vyama vya siasa;

ii. Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa Sura 258 na Sheria ya Gharama za Uchaguzi Sura 278;

iii. Kufuatilia michakato ya chaguzi na teuzi ndani ya vyama vya siasa;

iv. Kugawa ruzuku ya Serikali kwa vyama vya siasa vyenye sifa ya kupata ruzuku na kusimamia matumizi yake;

v. Kutoa miongozo na kufuatilia mapato na matumizi ya vyama vya siasa na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za chama;

vi. Kutoa elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria ya Gharama za Uchaguzi;

vii. Kuratibu elimu ya uraia inayotolewa kwa vyama vya siasa;

viii. Kuishauri Serikali katika masuala yanayohusiana na vyama vya siasa;

ix. Kuwezesha mawasiliano kati ya Serikali na Vyama vya Siasa;

x. Kufanya tafiti kuhusu vyama vya siasa na mfumo wa demokrasia ya vyama vingi nchini;

xi. Kusimamia Utekelezaji wa Kanuni za Kuratibu Mikutano ya Hadhara.

orpptanzania

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa
Viwanja vya Nanenane Nzuguni
Jengo la Wizara ya Kazi -
Mtaa wa Nzuguni A,
S.L.P 2851 DODOMA.

Tovuti yetu